**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAMBO YA RAIS NAMBA 5 YA 1993 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMBO YA RAIS KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI KUHUSIANA NA MAMBO YA RAIS NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### SHUGHULI ZA RAIS, KAZI, UWEZO NA KINGA

3. Kuanzishwa kwa Ofisi.
4. Kazi za Rais katika kuanzisha Wizara.
5. Uwezo wa Rais Kutoa tamko na Amri Rasmi ya Serikali.
6. Uwezo wa Rais kuhusiana na Siku za Mapumziko na dharura.
7. Uwezo wa Rais kukasimu kazi na majukumu yake.
8. Kinga.
9. Malipo ya Rais.

### SEHEMU YA TATU
### TUNZO

10. Tunzo.
11. Kamati ya Ushauri ya utowaji wa Tunzo.
12. Hati ya Tamko la Tunzo.
13. Tunzo ni mali ya Serikali.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

14. Uwezo wa Waziri kutunga kanuni.

15. Makosa na adhabu.

16. Adhabu ya jumla.

17. Kufuta na kubakiza.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 3 YA 2020**

**NIMESAINI**

Alhemin

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

5 Mei ........................................................, **2020**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAMBO YA RAIS NAMBA 5 YA 1993 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMBO YA RAIS KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI KUHUSIANA NA MAMBO YA RAIS NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mambo ya Rais, 2020 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Tunzo" inajumuisha zawadi ya kuthamini, zawadi ya heshima, nishani au kitu chochote kinachotolewa na Rais kwa kuthamini utumishi kwa mtu yeyote chini ya Sheria hii;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Ushauri iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria hii;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo yanayomuhusu Rais;

"Ofisi" maana yake ni Ofisi ya Faragha iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Wafanyakazi wa Rais" maana yake ni wafanyakazi wanaofanya kazi katika Ofisi ya Faragha ambao inajumuisha wasaidizi wa Rais kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Wasaidizi" inajumuisha Makamu wa Rais, Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Sheha, au mtumishi yeyote wa umma.

## SEHEMU YA PILI
## SHUGHULI ZA RAIS, KAZI, UWEZO NA KINGA

Kuanzishwa kwa Ofisi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Ofisi ya Faragha ya Rais.

(2) Rais atamteua mtu atakaemuona anafaa kuwa mfanyakazi wa Ofisi hiyo.

(3) Rais ataanzisha Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Rais na kuteua wafanyakazi wa Ofisi hiyo.

(4) Wafanyakazi wa Rais watastahiki kupata mshahara, posho, huduma na fursa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(5) Ofisi itatoa huduma kwa Rais kama itakavyohitajika kwa utekelezaji bora na wa ufanisi wa kazi za Rais.

Kazi za Rais katika kuanzisha Wizara.

**4.**-(1) Kwa kuzingatia Katiba au sheria nyenginezo, kuanzisha, kuondosha, kuunganisha na kupanga upya Wizara na Idara kutafanywa na Rais.

(2) Serikali itajumuisha Makamu wa Rais, Mawaziri, Watumishi wa Idara Maalum na watumishi wa umma na watawajibika kwa Rais.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, uteuzi wa mawaziri na wakuu wa idara utafanywa kwa mujibu wa ridhaa ya Rais.

(4) Itakuwa ni jukumu la kila Waziri katika Serikali kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Bajeti ya Wizara kwa Rais.

Uwezo wa Rais Kutoa tamko na Amri Rasmi ya Serikali.

**5.**-(1) Rais anaweza, kwa kuzingatia uwezo aliopewa kwa mujibu wa Katiba kuwa ni Mkuu wa Nchi na Mkuu wa Serikali, kutoa tamko na Amri Rasmi ya Serikali kwa kadri inavyostahiki kufanikisha kazi zake.

(2) Bila ya kujali sheria zozote, itakapotokea Rais kuridhika kwa mujibu wa mazingira yaliyopo kuwa ni muhimu kwake kuchukua hatua za haraka, anaweza kutoa tamko la kisheria kama ambavyo itatokea au kuhitajika kwa mujibu wa mazingira hayo, isipokuwa kwamba tamko hilo la kisheria lisiwe kinyume na Katiba.

Uwezo wa Rais kuhusiana na Siku za Mapumziko na dharura.

**6.**-(1) Bila ya kuathiri sheria nyengine zilizopo, Rais atakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kuteuwa siku yoyote kuwa ni siku ya mapumziko pale itakapoonekana ni muhimu kufanya hivyo; na

(b) kutangaza dharura pale litakapotokea janga ambalo linaweza kuathiri shughuli za Serikali au za watu.

(2) Siku itakayoteuliwa chini ya aya (a) au dharura itakayotamkwa chini ya aya (b) ya kifungu hiki, itatangazwa katika Gazeti Rasmi.

Uwezo wa Rais kukasimu kazi na majukumu yake.

**7.**-(1) Pale itakapotokea au kwa mujibu wa sheria zilizopo isipokuwa Katiba, kazi au jukumu lolote alilopewa Rais kutekeleza, utekelezaji wa kazi au jukumu hilo la Rais litaweza kutekelezwa na wasaidizi wake.

(2) Kifungu hiki hakitotumika katika uwezo wa Rais kuhusiana na uwezo wake wa kutoa matamko au uwezo wa Rais kwa nafasi yake akiwa Mkuu wa Nchi, isipokuwa tu kwa zile kazi ambazo sheria nyengine zinaeleza kuwa inawezekana kufanywa na maofisa wa Serikali.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya kazi au kutumia uwezo ambao ni mahsusi kwa Rais.

(4) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Kinga.

**8.**-(1) Rais ana kinga dhidi ya kushtakiwa kwa kosa la jinai au madai, kukamatwa, kutakiwa au kulazimishwa kufika au kuhudhuria yeye binafsi mahakamani, au kutakiwa au kulazimishwa kumleta mtu au kukileta kitu mahakamani.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, Rais hatokamatwa kwa kosa ambalo alilitenda wakati bado hajawa Rais na baada ya kumaliza muda wa uraisi au kutakiwa au kulazimishwa kufika au kuhudhuria yeye binafsi mahakamani, au kutakiwa au kulazimishwa kumleta mtu au kukileta kitu mahakamani.

Malipo ya Rais.

**9.** Kwa kila mwaka wa fedha, kutakuwa na malipo yatakayolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, malipo ambayo yataidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali ikiwa ni malipo kwa ajili ya mshahara, posho na matumizi mengine ya Rais.

## SEHEMU YA TATU
## TUNZO

Tunzo.

**10.**-(1) Rais anaweza kuanzisha na kutoa tunzo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Rais anaweza kutoa tunzo zifuatazo:

(a) Nishani ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964;

(b) Utumishi uliotukuka;

(c) Utumishi wa muda mrefu na Utiifu kwa Idara Maalum; na

(d) Ushujaa.

(3) Katika kutumia uwezo alionao chini ya kifungu hiki, Rais anaweza kutoa tunzo kwa kadri itakavyostahiki.

(4) Rais ataitangaza katika Gazeti Rasmi tunzo inayotolewa chini ya kifungu hiki kwa namna ilivyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii, ambayo inajumuisha jina la atakayetunukiwa tunzo, na vitu vilivyoundiwa tunzo.

(5) Nishani ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964 itakuwa ndiyo Nishani yenye hadhi ya juu.

Kamati ya Ushauri ya utowaji wa Tunzo.

**11.**-(1) Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya utowaji wa Tunzo ambayo Wajumbe na kazi zake zitakuwa kama inavyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

(2) Rais anaweza kushauriana na Kamati ya Ushauri kabla ya kutumia uwezo wake chini ya kifungu hiki.

Hati ya Tamko la Tunzo.

**12.** Tunzo itatolewa pamoja na Hati ya Tamko la Tunzo iliyosainiwa na Rais kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii.

Tunzo ni mali ya Serikali.

**13.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, tunzo zinazotolewa chini ya Sheria hii zitakuwa ni mali ya Serikali.

(2) Rais anao uwezo wa kuifuta tunzo yoyote inayotolewa chini ya Sheria hii endapo masharti ya tunzo hiyo yatavunjwa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

Uwezo wa Waziri kutunga kanuni.

**14.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi, kutunga kanuni kuelezea vigezo vya Tunzo vinavyoainisha sifa zinazohitajika kwa mtu atakaepewa tunzo chini ya kifungu cha 10 cha Sheria hii.

Makosa na Adhabu.

**15.** Mtu ambaye ataiharibu, ataivunja, ataibadilisha umbo, ataitoboa au ataitumia vibaya, tunzo yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Adhabu ya jumla.

**16.**-(1) Itakuwa ni kosa kuitumia vibaya au kwenda kinyume na kazi iliyokasimiwa au kuidharau kinga ya Rais iliyo chini ya Sheria hii.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Mbili au kutumikia kifungo kwa muda usiozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

Kufuta na kubakiza.

**17.**-(1) Sheria ya Mambo ya Rais Nam.5 ya 1993 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa chini ya Sheria iliyofutwa kitachukuliwa kuwa kimefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

## SHERIA YA MAMBO YA RAIS, Nam. 3 ya 2020

**TAARIFA**

**(Chini ya kifungu cha 10)**

---

**KWA KUWA** kifungu cha 10 cha Sheria ya Mambo ya Rais kinampa uwezo Rais **kuanzisha** na kutoa Tunzo;

**NA KWA KUWA** nimeridhika kwamba ni muhimu na ni jambo jema kuanzisha Tunzo kwa mtu ambaye, kwa kuzingatia umahiri wa vitendo au matendo yake anastahiki sifa hiyo na kutunzwa ili kuthibitisha kuyatambua hayo:

**HIVYO BASI,** Mimi,.................................... Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutumia uwezo wangu niliopewa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Mambo ya Rais, 2020, naeleza kuwa Tunzo iliyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Taarifa hii, ambayo atapewa mtu aliyeainishwa kuhusika na Tunzo hiyo. Utaratibu wa kukabidhi Tunzo hiyo utakuwa kama ulivyoainishwa hapa.

| TUNZO | | JINA | NISHANI (ASILI) |
|---|---|---|---|
| 1. | Nishani ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964 | 1.................<br>2. .............. | mf. Dhahabu. |
| 2. | Utumishi Uliotukuka | 1. ..............<br>2. .............. | |
| 3. | Utumishi wa muda mrefu na Utiifu kwa Idara Maalum | 1. ..............<br>2. .............. | |
| 4. | Ushujaa | 1. ..............<br>2. .............. | |

| Alama ya Nishani | Utaratibu wa kuvaa |
|---|---|
| 1. | .......................................... |
| 2. | .......................................... |
| 3. | .......................................... |

## JADWELI LA PILI

## WAJUMBE NA KAZI ZA KAMATI YA USHAURI

**[imefanywa chini ya kifungu cha 11(1)]**

---

**1.** Kamati ya Ushauri ya itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti, ambae atakuwa ni Waziri anayehusika na mambo ya Rais;

(b) Katibu Mkuu Kiongozi;

(c) Mwanasheria Mkuu;

(d) Kamanda wa Brigedia ya Nyuki; na

(e) Wajumbe wengine watatu walioteuliwa na Rais wenye sifa kwa madhumuni hayo kwa kuzingatia jinsia.

**2.** Kamati ya Ushauri itakuwa na kazi ya kumshauri Rais katika mambo yafuatayo:

(a) Katika kuchagua watu wenye sifa ya kupewa Tunzo yoyote katika Tunzo hizo;

(b) Alama na utaratibu wa kuvaa Nishani; na

(c) Katika mambo mengine yanayohusiana na Tunzo.

**3.** Sekretarieti ya Kamati ya Ushauri itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Mkuu anayeshughulikia mambo ya Rais atakuwa Katibu wa Kamati ya Ushauri na Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Kamati ya Ushauri;

(b) Katibu Mkuu kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(c) Katibu Mkuu kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

(d) Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi; na

(e) Naibu Mwanasheria Mkuu.

**4.** Sekretarieti ya Kamati itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kupanga vikao, kuhifadhi na kutunza kumbukumbu;

(b) kukusanya na kufanya upembuzi jina la mtu aliyependekezwa kupewa Tunzo lililowasilishwa katika Kamati;

(c) kuwezesha mawasiliano ya maamuzi na maelekezo ya Kamati; na

(d) kufanya kazi nyengine ambazo Kamati itaona zinastahiki kufanywa.

**JADWELI LA TATU**

**HATI YA TAMKO LA TUNZO**
**(imefanywa chini ya kifungu cha 12)**

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**KWA:**

..............................................................................

**SALAAM:**

**MIMI** ..........................................................................................................

**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAMBO YA RAIS NAM. 3 ya 2020**
**KWA KUUKUBALI MCHANGO WAKO KWA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR,**
**NIMEKUTUNUKU NISHANI YA** .......................

**IMETOLEWA IKULU PAMOJA NA MUHURI NA SAINI YANGU**

**TAREHE**

.....................................

**RAIS WA ZANZIBAR**
**NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 1 Aprili, 2020.

.....................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***